

# Nikupe Nini Ee Mungu Cha Kukupendeza

Na G A Chavallah  
Kurasini-Dar  
25-04-1998

1.Ni      ku pe ni ni EeMungu cha ku ku pe nde za      U      na wa u ju a Pa  
we zowangu m do go Bwa

mo ja na dhi ki i na yo ni so nnga Po      ngu hi i du ni  
ke a za wa di ya

2. Nikitazama wenzangu wanakutolea,  
Zawadi nyingi na nzuri za kukupendeza,  
Kasoro mimi tuu natoa kidogo,  
Wakati mwingine sito kabisa.
3. Maisha yangu ya dhiki Bwana wayajua,  
Unyonge na udhaifu wangu waujua,  
Sina kitu mimi cha kukutolea,  
Lakini pokea nafsi yangu Bwana.
4. Nayakabidhi maisha yangu kwako Bwana,  
Unionongoze katika njia ya uzima,  
Unisaidie wakati wa shida,  
Kwani ni wewe tuu tumaini langu.
5. Kutoa ndugu ni moyo sio utajiri,  
Ukimtolea Mungu atakuongeza,  
Uwasaidie watu masikini,  
Wasio jiweza utabarikiwa.
6. Ninawasihi wenzangu mlariojaliwa,  
Maisha bora mazuri na yakuridhisha,  
Msimsahau Bwana Mungu wenu,  
Toeni kwa wingi mtarikiwa.